



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

 **ewura**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

KUMB: PPR/2022 - 04/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 6 APRILI 2022

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Aprili 2022**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za rejareja na jumla za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Machi 2022. Kwa Aprili 2022, bei za rejareja za petroli, dizeli na mafuta ya taa zimeongezeka kwa shilingi 321/Lita (sawa na asilimia 12.65), shilingi 289/Lita (sawa na asilimia 12.04) na shilingi 473/Lita (sawa na asilimia 21.45), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za petroli, dizeli na mafuta ya taa zimeongezeka kwa shilingi 320.32/Lita (sawa na asilimia 13.29), shilingi 288.49/Lita (sawa na asilimia 12.69) na shilingi 472.40/Lita (sawa na asilimia 22.72), mtawalia.
- (b) Kwa Aprili 2022, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya petroli na dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimeongezeka ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 2 Machi 2022. Kwa Aprili 2022, bei za rejareja za petroli na dizeli zimeongezeka kwa shilingi 285/lita (sawa na asilimia 11.12) na shilingi 295/lita (sawa na asilimia 11.90), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za petroli na dizeli zimeongezeka kwa shilingi 284.22/Lita (sawa na asilimia 11.68) na shilingi 294.66/lita (sawa na asilimia 12.52) mtawalia. *Kutokana na kuisha kwa mafuta ya taa kwenye matanki ya kuhifadhiya yaliyopo Tanga, waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kuchukua mafuta ya taa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta ya taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.*
- (c) Kwa Aprili 2022, bandari ya Mtwara imepokea mafuta ya dizeli tu hivyo, kwa Aprili 2022 bei za rejareja na jumla za mafuta ya petroli kwa **mikoa ya Kusini**

(Mtwara, Lindi na Ruvuma) zitakuwa sawa na zile zilizotangazwa tarehe 2 Machi 2022. Kwa upande wa dizeli, kwa Aprili 2022, bei za rejareja na jumla za dizeli zimeongezeka ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita. Bei ya rejareja ya dizeli imeongezeka kwa shilingi 281/lita (sawa na asilimia 11.12) na bei ya jumla ya dizeli imeongezeka kwa shilingi 279.99/lita (sawa na asilimia 11.67). Kwa kuwa hakuna matanki ya kuhifadhi mafuta ya taa katika bandari ya Mtwara, *waendeshaji wa vituo vya mafuta kwenye mikoa ya Kusini wanashauriwa kuchukua mafuta ya taa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta ya taa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika*

- (d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za usafirishaji (*BPS Premium*) na thamani ya shilingi ukilinganisha na dola ya kimarekani.
- (e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (Price cap)** au **kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price)** kama ilivyokokotolewa kwa kutumia fomula na Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Magazeti ya Serikali Na. 2A na 57 ya tarehe 3 Januari 2022 na 28 Januari 2022, sawia.
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesa bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayooonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye

mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA (SHILINGI KWA LITA)

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	2,861	2,692	2,682
Arusha	2,905	2,836	2,766
Arumeru (Usa River)	2,905	2,836	2,766
Karatu	2,923	2,854	2,784
Longido	2,916	2,847	2,777
Monduli	2,910	2,842	2,771
Monduli-Makuyuni	2,915	2,846	2,776
Ngorongoro (Loliondo)	2,989	2,921	2,857
Coast (Kibaha)	2,866	2,697	2,686
Bagamoyo	2,872	2,703	2,693
Bagamoyo (Miono)	2,903	2,734	2,723
Chalinze Junction	2,876	2,706	2,696
Chalinze Township (Msata)	2,880	2,711	2,700
Kibiti	2,882	2,713	2,702
Kisarawe	2,869	2,699	2,689
Mkuranga	2,871	2,702	2,691
Rufiji	2,889	2,720	2,709
Dodoma	2,920	2,751	2,740
Bahi	2,927	2,758	2,748
Chamwino	2,915	2,746	2,736
Chemba	2,947	2,778	2,767
Kondoa	2,953	2,784	2,773
Kongwa	2,917	2,748	2,738
Mpwapwa	2,921	2,752	2,742
Mpwapwa (Chipogoro)	2,933	2,764	2,754
Mtera (Makatopora)	2,939	2,770	2,759
Mvumi	2,927	2,758	2,747
Geita	3,027	2,858	2,847
Bukombe	3,016	2,847	2,836
Chato	3,048	2,879	2,868
Mbogwe	3,065	2,896	2,885
Nyang'hwale	3,042	2,873	2,862
Iringa	2,926	2,756	2,746
Ismani	2,931	2,762	2,751
Kilolo	2,930	2,761	2,750
Mufindi (Mafinga)	2,936	2,766	2,756
Mufindi (Igowole)	2,944	2,775	2,764
Kagera (Bukoba)	3,077	2,908	2,897
Biharamulo	3,051	2,882	2,871

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Karagwe (Kayanga)	3,093	2,924	2,914
Kyerwa (Ruberwa)	3,099	2,930	2,919
Muleba	3,077	2,908	2,897
Ngara	3,065	2,896	2,885
Misenyi	3,085	2,916	2,906
Katavi (Mpanda)	3,069	2,900	2,890
Mlele (Inyonga)	3,089	2,920	2,909
Mpimbwe (Majimoto)	3,062	2,893	2,883
Tanganyika (Ikola)	3,087	2,918	2,908
Kigoma	3,093	2,924	2,913
Uvinza (Lugufu)	3,105	2,936	2,925
Buhigwe	3,082	2,913	2,902
Kakonko	3,050	2,881	2,870
Kasulu	3,079	2,910	2,899
Kibondo	3,057	2,888	2,877
Kilimanjaro (Moshi)	2,894	2,826	2,755
Hai (Bomang'ombe)	2,898	2,829	2,759
Mwanga	2,887	2,819	2,748
Rombo (Mkuu)	2,911	2,843	2,776
Same	2,881	2,812	2,742
Siha (Sanya Juu)	2,901	2,832	2,762
Lindi	2,691	2,825	2,741
Lindi-Mtama	2,696	2,829	2,759
Kilwa Masoko	2,715	2,849	2,715
Liwale	2,727	2,860	2,761
Nachingwea	2,711	2,845	2,770
Ruangwa	2,718	2,851	2,771
Manyara (Babati)	2,939	2,870	2,804
Hanang (Katesh)	2,949	2,881	2,815
Kiteto (Kibaya)	2,954	2,885	2,815
Mbulu	2,952	2,883	2,817
Simanjiro (Orkasumet)	2,971	2,902	2,836
Mara (Musoma)	3,040	2,871	2,860
Musoma Vijijiini (Busekela)	3,081	2,912	2,901
Rorya (Ingirijuu)	3,049	2,880	2,869
Rorya (Shirati)	3,084	2,915	2,904
Bunda	3,031	2,862	2,851
Bunda (Kisorya)	3,041	2,872	2,861
Butiama	3,037	2,868	2,857
Serengeti (Mugumu)	3,086	2,917	2,906
Tarime	3,051	2,882	2,871
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	3,056	2,886	2,876
Mbeya	2,969	2,799	2,789
Chunya	2,978	2,809	2,798
Chunya (Makongolosi)	2,983	2,814	2,804
Chunya (Lupa Tingatinga)	2,985	2,816	2,805
Kyela	2,984	2,815	2,805
Mbarali (Rujewa)	2,953	2,783	2,773
Rujewa (Madibira)	2,966	2,797	2,786
Rujewa (Kapunga)	2,962	2,793	2,783
Rungwe (Tukuyu)	2,978	2,808	2,798
Morogoro	2,886	2,717	2,707
Mikumi	2,902	2,733	2,722

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Kilombero (Ifakara)	2,924	2,755	2,744
Kilombero (Mlimba)	2,947	2,778	2,767
Kilombero (Mngeta)	2,936	2,767	2,756
Ulanga (Mahenge)	2,935	2,766	2,755
Malinyi	2,945	2,776	2,765
Kilosa	2,905	2,736	2,725
Gairo	2,905	2,736	2,725
Mvomero (Wami Sokoine)	2,897	2,728	2,717
Mvomero (Sanga Sanga)	2,886	2,717	2,707
Turian	2,912	2,742	2,732
Mtwara	2,678	2,811	2,754
Nanyumbu (Mangaka)	2,714	2,847	2,803
Masasi	2,694	2,827	2,780
Newala	2,698	2,832	2,786
Tandahimba	2,692	2,825	2,779
Nanyamba	2,692	2,825	2,779
Mwanza	3,012	2,842	2,832
Kwimba	3,029	2,860	2,850
Magu	3,020	2,850	2,840
Misungwi	3,006	2,837	2,826
Sengerema	3,044	2,875	2,864
Ukerewe	3,071	2,902	2,891
Njombe	2,954	2,785	2,774
Njombe (Kidegembye)	2,975	2,805	2,795
Ludewa	2,992	2,823	2,812
Makambako	2,946	2,777	2,766
Makete	2,985	2,816	2,805
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,952	2,782	2,772
Rukwa (Sumbawanga)	3,034	2,865	2,855
Sumbawanga Rural (Mtownisa)	3,034	2,865	2,855
Kalambo (Matai)	3,042	2,872	2,862
Nkasi (Namanyele)	3,048	2,879	2,868
Ruvuma (Songea)	2,763	2,897	2,805
Mbinga	2,776	2,909	2,839
Namtumbo	2,754	2,888	2,834
Nyasa (Mbamba Bay)	2,801	2,935	2,849
Tunduru	2,729	2,862	2,864
Shinyanga	2,991	2,822	2,811
Kahama	3,004	2,835	2,824
Kishapu	3,019	2,850	2,839
Ushetu (Nyamilangano)	3,022	2,852	2,842
Ushetu (Kangeme Village)	3,012	2,843	2,833
Salawe	3,005	2,836	2,825
Simiyu (Bariadi)	3,032	2,863	2,852
Busega (Nyashimo)	3,025	2,856	2,845
Itilima (Lagangabilili)	3,035	2,866	2,855
Maswa	3,023	2,854	2,843
Meatu (Mwanhuzi)	3,030	2,861	2,851
Singida	2,952	2,783	2,772
Iramba	2,964	2,795	2,784
Manyoni	2,937	2,768	2,757
Itigi (Mitundu)	2,952	2,783	2,772
Ikungi	2,948	2,778	2,768

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mkalama (Nduguti)	2,977	2,808	2,797
Songwe (Vwawa)	2,978	2,809	2,798
Songwe (Mkwajuni)	2,985	2,816	2,805
Ileje	2,982	2,813	2,802
Momba (Chitete)	2,987	2,818	2,807
Tunduma	2,982	2,813	2,802
Tabora	2,970	2,800	2,790
Igunga	2,969	2,800	2,790
Kaliua	2,983	2,814	2,803
Ulyankulu	2,980	2,811	2,800
Nzega	2,980	2,811	2,800
Sikonge	2,979	2,809	2,799
Urambo	2,980	2,810	2,800
Uyui	2,976	2,807	2,796
Mpyagula	3,001	2,832	2,821
Tanga	2,848	2,779	2,728
Handeni	2,869	2,800	2,707
Kilindi	2,884	2,815	2,742
Korogwe	2,860	2,792	2,721
Lushoto	2,870	2,801	2,730
Mkinga (Maramba)	2,855	2,787	2,742
Muheza	2,853	2,784	2,728
Pangani	2,855	2,786	2,734

JEDWALI B: BEI ZA JUMLA (SHILINGI /LITA)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar Es Salaam	2,730.50	2,561.45	2,551.48
Tanga	2,717.25	2,648.46	-
Mtwara	2,546.97	2,680.12	-

Mha. Godfrey H. Chibulunje
KAIMU MKURUGENZI MKUU- EWURA